



ARUSHA GATEWAY COLLEGE
S.L.P 3060 ARUSHA
Phone: 0757661770/ 0784661770
Email: arushagatewaycollege@gmail.com



**FOMU YA KUJIUNGA NA ARUSHA GATEWAY COLLEGE KWA MWAKA
WA MASOMO 2021/2022**

Ndg.

YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA

.....

Hongera sana

Ninafuraha kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga na mafunzo tajwa hapo juu ngazi ya cheti. Mafunzo hayo ni ya mwaka mmoja ambayo yatakuwezesha kupata cheti katika fani hiyo.

Cheti hicho kitapatikana baada ya kushiriki mafunzo kikamilifu darasani na mafunzo kwa vitendo (practical works)

ZINGATIA: Lugha ya kiingereza na Kispanyiola ni bure.

MAHITAJI YA MOJA KWA MOJA YA MWANAFUNZI (Direct cost)

- ✓ Fedha za tahadhari **50,000/=** kwa wanafunzi wa hostel tu.
- ✓ Kitambulisho **10,000/=**
- ✓ Matibabu **50,400/=** (Bima ya Afya)
- ✓ Sare za chuo **70,000/=** zinapatikana chuoni pamoja na T-shirt ya Chuo
- ✓ Mtihani wa Taifa Tsh **75,000/=** (**National examination Fees**)

ZINGATIA: Fedha tajwa hapo juu zilipwe kama ilivyoainishwa kwa muhula husika

**MCHANGANUO WA GHARAMA ZA MASOMO KWA MWAKA
MZIMA KWA MWANAFUNZI LA**

MUHULA WA KWANZA	MUHULA WA PILI
Hostel 90,000/=	Hostel 90,000/=
Ada 450,000/= kwa muhula	Ada 450,000/= kwa muhula
Chakula bure	Chakula bure
Godoro 35,000/=	Godoro 35,000/=

ZINGATIA: Kwa wanafunzi wa kutwa (Day students) hawatahusika na gharama za hostel

Fedha zote zilipwe kwenye akaunti ya Chuo Benki ya **POSTA (TPB)**
Jina la Akaunti. **Arusha Getway College**
Namba ya Akaunti. **215227000002**

MAHITAJI kwa wanafunzi wa hostel

- a) Blanket 2
- b) Sahani, bakuli, kijiko na kikombe
- c) Shuka za blue bahari awe msichana au mvulana
- d) Ndoo mbili ndogo , safari boot za kaki kwa wanachuo wa kozi ya utalii

MAHITAJI YA KITAALUMA.


Tafadhali ambatanisha fomu hii pamoja na cheti ya kuhitimu kidato cha nne au kidato cha sita kama kipo.

SARE ZA CHUO.

Zinapatikana chuoni kwa shilingi elfu sabini (Tsh. 70,000/=)

MAHALI CHUO KILIPO.

Chuo kipo Jiji la Arusha karibu na Round About ya Njiro East Africa Road



SHERIA NA KANUNI ZA CHUO

- 1) Wanachuo anapaswa kuwa na nidhamu kwa kipindi chote atakapokuwachuoni
- 2) Mwanachuo ambaye atashindwa kuheshimu sheria za chuo atasimamishwa masomo kwa mda wa miezi mitatu au kufukuzwa chuo kabisa
- 3) Wanachuo wote wanapaswa kuvaa sare za chuo mda wote wakiwa chuoni hasa kwenye vipindi vyao
- 4) Kila mwanachuo anapaswa kuwa na bima ya Afya kipindi awapo chuoni
- 5) Kila mwanachuo anapaswa kufanya mazoezi ya kitaaluma ya vitendo na darasani. Mwanafunzi atakayeshindwa kufanya mazoezi hayo hataruhusiwa kufanya mtihani wa mwisho (Taifa)
- 6) Kila mwanachuo anapaswa kupata **Continuous Assessment (CA)** ya 16 ili aweze kufanya mtihani wa mwisho.
- 7) Kila mwanachuo anapaswa kuingia kipindi cha dini chuoni kwa kila dhehebu lake
- 8) Migomo, matusi na kupigana ni kosa ambalo litakufukuzisha chuo
- 9) Kuvaa mavazi yasiyo ya heshima hairuhusiwi chuoni na nje ya chuo
- 10) Kila mwanachuo anapaswa kumheshimu mwanafunzi mwenzake, Viongozi na kuwa na ushirikiano ili kufikia malengo yake
- 11) Kila mwanachuo anapaswa kuwa na kitambulisho cha chuo, baada ya wiki moja kufika chuoni.
- 12) Kila mwanachuo anatakiwa kuwa na raba pamoja na nguo za michezo
- 13) Kila mwanachuo wa **Utalii** na **Hotel** anapaswa kushiriki kila ziara ya kimasomo katika baadhi ya mbuga za wanyama hapa nchini ili kujifunza kwa vitendo.
- 14) Kila mwanafunzi anapaswa kulipa Tsh **5,000/=** ya **Arusha Getway College Student's Organization (AGCSO)**

MAKOSA ATAKAYOFANYA MWANACHUO NA KUSABABISHA KUFUKUZWA CHUO

1. Uvutaji Bangi
2. Uasherati
3. Ulevi
4. Wizi
5. Kutokuhudhuria vipindi bila ruhusa ya mtaaluma
6. Kupigana na mwalimu au mfanyakazi wa chuo au na mwanachuo mwenzake
7. Kukataa au kutokushiriki katika ziara mbalimbali za kimasomo
8. Kuacha au kukataa kufanya mtihani
9. Kuharibu kwa makusudi mali ya shule au ya mwalimu
10. Kupatikana na kosa lolote la kijinai
11. Kuanzisha mgomo wa aina yoyote chuoni au nje ya chuo
12. Kuwa na mahusiano ya kimapenzi na Mwalimu au mwanafunzi
13. Kutokuvaa sare za chuo bila ruhusa ya mkuu wa Chuo au mtaaluma wa Chuo.
14. Kukataa kufuata agizo la mkuu wa Chuo au Mwalimu
15. Kuvaa nguo ambazo haziruhusiwi chuoni Kama vile kimini, Skini taiti na kitop